TANGAZO LA SERIKALI Na. 671 La Tarehe 21/8/2020

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

(I*metungwa chini ya kifungu 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO ZA ADA NA USHURU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI ZA MWAKA 2020

## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi za Mwaka 2020.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-

“ada” maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni zitolewazo na Halmashauri;

“Afisa Mwidhiniwa” maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

“boti” maana yake ni chombo cha majini kinachoendeshwa kwa kutumia injini iliyopachikwa au kujengewa ndani ya chombo hicho;

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi;

“kibali” maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

“machinjio” maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi;

"maegesho" maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha vyombo vya usafiri kwa muda;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mtumbwi" maana yake ni chombo cha majini kinachoendeshwa kwa kutumia joshi, mashine au kasia;

"tenga" maana yake ni kifaa chochote ikijumuisha ndoo, debe au kifaa chochote cha kiasili kinachotumika kupima au kubebea samaki au mazao ya majini;

*"ushuru"* maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala wake kwa ajili ya huduma zitolewazo na Halmashauri;

*"wakala"* maana yake ni mtu, taasisi, kampuni au asasi yoyote iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri;

## SEHEMU YA PILI
## UTARATIBU WA KUKUSANYA ADA NA USHURU

Utozaji wa ada na ushuru

4. (1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma zitolewazo na Halmashauri kama inavyoonyeshwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada itozwayo chini ya Sheria Ndogo hizi italipwa kabla ya huduma kutolewa.

(3) Ushuru utozwao chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kwa saa au siku au kabla ya kupata huduma au wakati wa kupata huduma.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

5. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

Muda wa kukusanya ada na ushuru

6. (1) Muda wa kukusanya ada na ushuru utakua kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi anaweza kukusanya ushuru baada ya muda uliotajwakatika kifungu kidogo cha (1).

(3) Malipo ya ada na ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Uteuzi wa wakala

7. Halmashauri inaweza kuteua kampuni, asasi au taasisi yoyote kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri.

Usimamizi wa Sheria Ndogo

8. (1) Halmashauri inaweza kufunga biashara au kusimamisha uendeshaji wa shughuli yeyote ambayo itafanyika bila kuwa na leseni au kibali kinachotelewa na Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha kidogo cha (1) wakala anaweza kukamata au kutumia mali au bidhaa za mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipa ushuru kwa mujibu wa masharti ya Sheria Ndogo hizi.

(3) Endapo mmiliki wa mali za bidhaa iliyokamatwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) atashindwa kulipa ushuru unaodaiwa ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya Mahakama itakuwa na mamlaka ya kuuza mali au bidhaa hizo na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mali au bidhaa hizo baada ya kutoa ushuru unaodaiwa, gharama za kuhifadhi mali au bidhaa, gharama za Mahakama na gharama za mnada.

(4) Wakala hataruhusiwa kukamata mali au bidhaa bila idhini ya maandishi ya Mkurugenzi.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu au hasara yoyote itakayotokea kutokana na utekelezaji wa Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama uharibifu utasababishwa na Halmashauri au Wakala.

Ukaguzi

9. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa:
   (a) kuingia katika muda ulioruhusiwa na Sheria Ndogo hizi kwenye jengo lolote kwa lengo la kukusanya ushuru; na
   (b) kukagua eneo au chombo chochote atakachokitilia mashaka kuwa kinahifadhi au kusafirisha bidhaa au kinatumika kukwepa kulipa ushuru.

## SEHEMU YA TATU
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa

10. (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:
   (a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;
   (b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa ada au ushuru;
   (c) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri au shughuli zinazohitaji kulipiwa ushuru;
   (d) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au wakala kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hizi.

   (2)Endapo mtu yeyote atapatikana na hatia chini ya kifungu kidogo cha (1) atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

11. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote kiasi cha shilingi elfu thelathini iwapo mtu huyo atakiri kosa kwa hiari na kujaza fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi na kukubali kutekeleza wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi.

Kufutwa Tangazo la Serikali Na. 257 la mwaka 2018

12. (1) Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi za Mwaka 2018 zinafutwa.

   (2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), ada na ushuru unaodaiwa na Halmashauri utaendelea kudaiwa chini ya Sheria Ndogo hizo.

*Tangazo la Serikali Na. 671 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kifungu 4(1)*

A: USHURU WA MAEGESHO

I. Ushuru wa maegesho ya mitumbwi
1.Mitumbwi………. 200 /= kila unapoegeshwa kwa siku
2. Kalua/Ngama….. 500 /= kila inapoegeshwa kwa siku
3. Kivuko 'Ferry'…. 500/= kila inapoegeshwa kwa siku
4. Meli Ndogo……. 2,000/= kila inapoegeshwa kwa siku
5. Boti iliyobeba sanduku za kubeba
samaki……………. 1,500/= kila inapoegeshwa kwa siku
6. Makontena……… 5,000/= kila inapoegeshwa kwa siku
7. Mitumbwi ya kusafirisha abiria……… 500 /= kila safari

II. Ushuru wa maegesho ya magari ya biashara kwenye magulio, mialo na masoko

1. Gari lenye tani 1-7…… 2,000/= kwa siku
2. Gari lenye tani 8-10…… 5,000/= kwa siku
3. Gari la zaidi ya tani 10… 10,000/= kwa siku
4. Pikipiki…………………… 500/= kwa siku
5. Magari binafsi yasiyo ya biashara.. 500/= kwa siku

B. USHURU WA MAZAO YA KILIMO NA MAZAO YA MAJINI

I. Bidhaa za kilimo
Mazao yote ya chakula na biashara ndani ya Halmashauri yanayozidi uzito wa tani moja yatalipiwa ushuru wa asilimia (3%) ya bei ya mauzo.

II. Bidhaa za Majini

1. Kilo moja ya samaki wabichi mwaloni…………………………… 100/= kwa kilo
2. Samaki wakavu:
   (i) tenga la kawaida la samaki wakavu (chini ya samaki 60) ……. 2,000/=
   (ii) tenga kubwa la samaki wakavu (zaidi ya samaki 60)…………. 5,000/=

3. Dagaa
   (i) Gunia dogo la dagaa (chini ya kilo 54) ………………………. 2,000/=
   (ii) Gunia la kubwa dagaa (zaidi ya kilo 54)…………………….. 3,000/=

4. Gunia la magamba ya konokono:
   kg 1-20 …………………………………………………….. 500/=
   kg 21-50……………………………………………………. 1,000/=

5. Mabondo ………………………………………………………… 2,000/= kwa kilo

6. Chakula cha Mifugo:
   kg 1-20…………………………….…………………… 500 /=

*Tangazo la Serikali Na. 671 (Linaendelea.)*

kg 21-50 ……………………………………………………..… 800/=
kg 51-100………………………………………………….…. 1,000 /=

7. Mabini ya samaki…………………………………………............ 1,000/= kila tani kwa safari

C. USHURU NDANI YA MASOKO, MAGULIO NA MIALO KWA SIKU

1. Biashara ya nguo za mitumba…………. 1,000/=
2. Biashara ya nguo za maduka………….. 1,000/=
3. Biashara ya viatu vya mitumba………. 1,000/=
4. Biashara ya mamalishe………………… 1,000/=
5. Biashara ya vileo………………………. 1,000/=
6. Biashara ya kuuza nyama……………… 5,000/=
7. Michezo mbalimbali……………………. 2,500/=
8. Biashara za bidhaa za urembo………….. 1,000/=
9. Biashara ya vyombo vya ndani……….... 1,000/=
10. Biashara ya samani mbalimbali…………. 1,000/=
11. Mazao ya kilimo kwa gunia/tenga ……… 2,000/=
12. Biashara ambazo hazijatajwa……………. 2,000/=

D. USHURU WA MAZAO YA MISITU

1. Gunia la Mkaa ………………………………. 1,000/=
2. Mbao…- 500/=kila ubao uziozidi futi 12 za 1x8, 1x10, 2x3, 2x6
   - 300/= kila ubao wenye vipimo vya 2x2,1x4 kwa urefu usiozidi futi 12……..300/=
   - kila futi itakayoongezeka Tsh.50/=
3. Kuni… - Tani 1-5 Tsh. 30,000/=
   - Tani 5-10 Tsh.50,000/=
   - zaidi ya Tani 10 Tsh. …. 1,000/= kwa kila tani itakayoongezeka.
4. Nguzo……………………………. 300/=kila moja
5. Gogo…………………………….. 3,000/= Kila mita za ujazo
6. Fito… - Tani 0-5 ……………. 20,000/=
   - Tani 6-10………….. 30,000/= na Tsh.500/= kwa kila Tani itakayoongezeka
7. Asali……….. …………………….. 500/= kila lita tano za ujazo
8. Nta………………………………… 500/=kwa kila kilo
9. Kibali cha kukata mti au kuvuna mti.. 1,000/=Kila mti
10. Mabanzi…………………………… 200/= kila moja

E. ADA ZA SHUGHULI ZA BURUDANI NA TIBA MBADALA

1. Disco za siku za kawaida, sikukuu na mwisho wa juma ……………………………………………………….. 20,000/= kwa siku
2. Waganga wa jadi………………………………………… 50,000/= kwa mwaka
3. Taasisi yoyote…………………………………………… 100,000/= kwa mwaka
4. Michezo ya sanaa za maonyesho ngoma, maigizo,sarakasi, michezo ya nguvu, nyimbo 5,000./= kwa siku katika taasisi na Tsh………..10,000/= kwa siku katika kumbi
5. Shughuli za sanaa za ufundi (uchoraji) picha, upakaji rangi, vinyago…..10,000/= kwa onyesho
6. Kunasa kanda za sauti kwa vikundi wakati wa mashindano ama shughuli iliyoandaliwa na Halmashauri ……………………………………….. 10,000./= kwa siku
7. Vikundi vya sanaa za ufundi ……………………… 10,000/= kwa mwaka.
8. kuendesha promotion/matangazo katika bar/hotel/maeneo ya wazi 20,000/= kwa siku

*Tangazo la Serikali Na. 671 (Linaendelea.)*

9. wasambazaji wa cable za runinga (TV) ……………. 30,000./= kwa mwezi
10. Kucheza meza za pool……………………………… 10,000/= kwa mwezi
11. Utundikaji wa matangazo ya vitambaa kwenye barabara…… 2 ,000/= kwa mwezi
12. Utundikaji wa matangazo ya karatasi……………………… 10,000 kwa mwezi

13. Sehemu za makumbusho au za kihistoria kwa mtu mmoja:
    i. Mtu mzima raia ……1,000 /=
    ii. Mtu mzima asiye raia ……Us $ 10
    iii. Mwanafunzi wan je ya nchi …….Us $ 5
    iv. Mwanafunzi wa ndani ya nchi…Bure

14. Kuendesha utafiti wa mambo ya kale na tafiti nyingine zinazofanana na hizo kwa miezi mitatu:
    i. Raia 50,000/=
    ii. Asiye raia Us $ 70

F. ADA NA USHURU WA MIFUGO

1. Ada ya machinjio

| | Machinjioni | Maeneo maalum (slaughter slub) kwa kila mfugo |
|---|---|---|
| Ng'ombe | 3,500/= | 2,000/= |
| Nguruwe | 2,000/= | 1,000/= |
| Mbuzi | 2,000/= | 1,000/= |
| Kondoo | 2,000/= | 1,000/= |

2. Ada ya jengo la kutunza ngozi kwa mwezi……………………………… 30,000/=

3. Ushuru wa Mifugo (mnadani)

Aina ya mifugo

Ngombe………………………………………… . 4,000/= kila mmoja
Mbuzi/kondoo…………………………………… 1,000/=kila mmoja
Nguruwe …………………………………………. 1,000/=kila mmoja

G. ADA YA VIBALI VYA UJENZI

1. Kibali cha ujenzi kwa ajili ya nyumba ya makazi …………………. 400/= kwa $M^2$
2. Kibali cha ujenzi kwa ajili ya nyumba ya makazi na biashara……… 500/= kwa $M^2$
3. Kibali cha ujenzi kwa ajili ya jengo la biashara/kituo cha mafuta …. 600/= kwa $M^2$

H. ADA YA UKAGUZI WA AFYA

1. Nyumba za starehe (baa, vilabu vya pome za kienyeji na nyumba za kulala wageni) …..5,000/= kila baada ya miezi sita
2. Ukaguzi wa wahudumu wa vyakula…………………………. 5,000/= kila baada ya miezi sita
3. Maduka ya bidhaa…………………………… 5,000/= kila baada ya miezi sita

*Tangazo la Serikali Na. 671 (Linaendelea.)*

4. Nyumba za kutengeneza na kuuzia vyakula na nyama choma… 5,000/=kila baada ya miezi sita
5. Ukaguzi wa maombi ya kufungua biashara…………. 10,000/= kila ombi
6. Ukaguzi wa maombi ya kufungwa biashara baada ya ukaguzi ili kufunguliwa upya 25,000/=.kila ombi
7. Ukaguzi wa viwanda vikubwa………………… 150,000/= kwa mwaka
8. Ukaguzi wa viwanda vya kati…………………. 100,000/= kwa mwaka
9. Ukaguzi wa viwanda vidogo………………….. 50,000/= kwa mwaka
10. Bucha …………………………………………. 5,000/= kwa mwaka
11. Machinjio……………………………………… 5,000/= kwa mwaka
12. Saluni…………………………………………. 2,000/= kwa mwaka

I. USHURU WA VIBAO VYA MATANGAZO YA BIASHARA

Kila tangazo la biashara litalipia Tsh. 1,000/= kwa kila $M^2$

J. ADA NA USHURU WA ARDHI

1. Mabadiliko ya Makazi kuwa biashara……………… 20,000/=
2. Mabadiliko ya biashara kuwa viwanda…………… 20,000/=
3. Mabadiliko ya makazi kuwa biashara ……………… 20,000/=
4. kugawanya kiwanja au shamba…………………….. 25,000/=
5. kuhakiki milki……………………………………… 25,000/=
6. kibali cha mauziano ya ardhi na viwanja………….. Tsh. 10,000/= kwa kila mauziano ya ardhi yenye thamani chini ya Tsh. Milioni mia moja na Tsh. 40,000/= kwa mauziano ya ardhi yenye thamani ya zaidi ya milioni mia moja.
7. ushuru wa mauziano ya ardhi………………………. Mauziano baina ya mtu na mtu au baina ya Serikali ya Kijiji na mtu binafsi yatalipiwa 10% ya mauzo kwa Halmashauri ya wilaya

Mgawanyo wake utakuwa kama ifuatavyo:
i. Halmashauri ya wilaya itapata 10% ya thamani ya mauzo ya ardhi;
ii. kijiji kitapata 10% ya kiasi ilichopata Halmashauri;
iii. kata husika itapata 10% ya kiasi ilichopata Halmashauri

K. USHURU MWINGINE

1. Molasses…………………………………………… 20/= kwa kila lita
2. Ushuru wa mnada wa jumla wa kitu kinachonadiwa… 5% ya bei ya mnada
3. Choo cha umma……………………………………… 300/= kila anapoingia
4. Kibali cha kufyatua matofali ……………………….. 20,000/= kwa miezi sita
5. Gari la kusomba mbolea Tani 1-8…………………... 3,000/= kwa safari
6. Gari la kusomba mbolea Tani 9-18………………….. 5,000/= kwa safari
7. Gari la kusomba mbolea Tani 19 nakuendelea………. 7,000/= kwa safari
8. Gari lenye maganda ya kahawa Tani 1-8……………... 3,000/= kwa safari
9. Gari lenye maganda ya kahawa Tani 9-18……………. 5,000/= kwa safari
10. Gari lenye maganda ya kahawa Tani 19 nakuendelea … 7,000/= kwa safari
11. Gari la mabaki ya mbao zilizochunwa (papara)…………10,000 kwa safari

*Tangazo la Serikali Na. 671 (Linaendelea.)*

12. Gari kubwa lenye nyasi za kuezeka Tani 9 nakuendelea..50,000/= kwa safari
13. Kupakia au kupakua bidhaa za viwandani tani 1-4……..10,000/= kwa safari
14. Kupakia au kupakua bidhaa za viwandani tani 5 nakuendelea…15,000/= kwa safari
15. Gari la mafuta ya taa, dizeli au petrol chini ya tani 10…...20,000/= kwa safari
16. Gari la mafuta ya taa, diseli au petrol zaidi ya lita 10……25,000/= kwa safari
17. Gari la gesi na bidhaa nyingine za mlipuko ……………..30,000/= kwa safari

L. ADA MBALIMBALI

1. Ada ya Kibali cha kufyatua matofali……………………… 20,000/= kwa miezi sita
2. Ada ya usajili wa vikundi…………………………………. 15,000/= kwa usajili
3. Ada ya kikundi kilichosajiliwa…………………………….. 10,000/= kwa mwaka

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 11)*

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi…………………………nakiri mbele ya ……………………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, kwamba tarehe…..ya mwezi……………mwaka ………nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha …………………cha Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi za mwaka 2020.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, kwa hiari yangu niko tayari kulipa kiasi cha shilingi elfu thelathini na kulipa ada/ushuru unaodaiwa.

NATHIBITISHA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU NA UFAHAMU WANGU.

Leo tarehe………..ya mwezi………….mwaka…………..
Jina:………………………………..
Saini:……………………………….

Mbele ya:
Jina:…………………………………….
Cheo:…………………………………
Saini:…………………………………

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa katika Kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi kilichofanyika tarehe 08/11/2019 na tarehe 09/11/2019 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya-

PROJESTUS K. TEGAMAISHO
*Mwenyekiti*
*Halmashauri Ya Wilaya Ya Misenyi*

INNOCENT M. MUKANDALA
*Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Wilaya*
*Missenyi*

S.L

NAKUBALI

Dodoma
5 Agosti, 2020

SELEMANI S. JAFO (MB),
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,*
*Tawala za Mikoa na Serikali za*
*Mitaa*